TANGAZO LA SERIKALI NA. 255 la tarehe 17/4/2024

SHERIA YA USIMAMIZI NA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128*)

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA MAGARI MATANO KWA MRADI WA KASKAZINI WA USAID-AFYA YANGU WA TAASISI YA ELIZABETH GLASER PEDIATRIC AIDS FOUNDATION YA MWAKA 2024

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Magari Matano kwa Mradi wa Kaskazini wa USAID-Afya Yangu wa Taasisi ya Elizabeth Glaser Pediatric Aids Foundation ya Mwaka 2024 na itachukuliwa kuwa ilianza kutumika tangu tarehe 22 Februari, 2024.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachotakiwa kulipwa kwa magari matano yaliyoanishwa kwenye Jedwali, yanayoingizwa au kununuliwa ndani au nje ya nchi kabla ya kibali cha forodha na Taasisi ya Elizabeth Glaser Pediatric AIDS Foundation kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Kaskazini wa USAID-Afya Yangu, kimesamehewa.

Masharti

3. Msamaha wa kodi unaotolewa chini ya Amri hii utafika ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba msamaha chini ya Amri hii haukutolewa, iwapo magari husika yatatumika kwa matumizi tofauti au yatahamishwa, kuuzwa au kwa namna yoyote atapewa mtu mwingine asiyestahili kufaidika na faida zinazotolewa chini ya Amri hii.

Kuisha kwa muda

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafika ukomo tarehe 21 Agosti, 2024.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na | Maelezo | Namba ya Chasis | Namba ya Injini |
|---|---|---|---|
| 1. | Toyota Land Cruiser Hardtop yenye uwezo wa kubeba watu 10, yenye milango 5 | JTEEB71J80F022417 | IHZ-1026641 |
| 2. | Toyota Land Cruiser Hardtop yenye uwezo wa kubeba watu 10, yenye milango 5 | JTEEB71J70F022425 | IHZ-1026745 |
| 3. | Toyota Land Cruiser Hardtop yenye uwezo wa kubeba watu 10, yenye milango 5 | JTEEB71JX0F022547 | IHZ-1027751 |
| 4. | Toyota Land Cruiser Hardtop yenye uwezo wa kubeba watu 10, yenye milango 5 | JTEEB71J30F022552 | IHZ-1027770 |
| 5. | Toyota Land Cruiser Hardtop yenye uwezo wa kubeba watu 10, yenye milango 5 | JTEEB71J50F022567 | IHZ-1027901 |

Dodoma,
28 Machi, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*